# LEARNING BY EAR 2012

## “Bado ningali mwanadamu- Riwaya inayoangazia matatizo yanayowapata watu wanaougua maradhi ya akili barani Afrika”

## EPISODE 2: “Mateso yasioweza kuelezeka”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: KAPAKA NYUMBANI KWAKE BAADA YA KUPOTEZA KAZI**

- **Kapaka (mume, 25)**
- **Cheupe (mke, 25)**
- **Msimulizi**

**SCENE TWO: VALERIE NA IRENE CHUMBANI CHUONI**

- **Valerie (mke, 19)**
- **Irene (mke, 19)**
- **Msimulizi**

**SCENE THREE: MALEMBA NA CHUMBA KATIKA KLINIKI YA MTAANI**

- **Malemba (mke, 35)**
- **Chumba (mume, 16)**
- **Matilda (mke, 40)**
- **Msimulizi**

**<u>SCENE FOUR: KAPAKA NA CHEUPE NYUMBANI KWAO</u>**

- **Kapaka (mume, 25)**
- **Cheupe (mke, 25)**

**<u>UTANGULIZI:</u>**

Nakusalimu na karibu katika hadithi ya **“Bado ningali mwanadamu”,** ikiwa ni makala ya **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Kipindi cha redio kinacholetwa kwako na Deutsche Welle. Riwaya hii ni kuhusu matatizo yanayowapata watu wanaougua maradhi ya akili barani Afrika. Kipindi cha kwanza, Kapaka alifukuzwa kazi katika duka la jumla. Valerie, mwanafunzi wa uuguzi hajaacha kumshangaza rafikiye Irene, kwa vituko vyake walipokuwa wakila chakula cha mchana. Na kule kijijini, Malemba akijizatiti kufukuza mapepo wanaomsababishia mwanae Chumba kupiga kelele zisizoeleweka. Hadithi hii itatupeleka wapi? Using’atuke, tusikilize kipindi hiki cha pili kwa jina, **“Mateso yasioweza kuelezeka”.** Tunaanza na Kapaka akiwasili kwake mapema, kuliko inavyotarajiwa. Anasubiriwa na mkewe mjamzito, Cheupe.

**<u>SCENE ONE: KAPAKA NYUMBANI BAADA YA KUFUKUZWA KAZI</u>**

1. **ATMO: AT KAPAKA’S HOME**

2. **SFX:** **DOOR BEING OPENED AND LOCKED**

3. **CHEUPE:** **(surprised)** Kapaka! Leo mbona kaja mapema. Kwani umenikosa sana hivyo?

4. **KAPAKA:** **(complaining)** La, si mimi …

5. **CHEUPE:** **(teasing)** Hukunikosa? Hiyo inauma kwa sababu mimi saa zote hutamani kuwa nawe.

6. **KAPAKA:** Sijawahi, husikii nisemacho? Haikuwa mimi! Sio sawa! Sio haki!

7. **CHEUPE:** Kapaka, kuna shida gani? Kumetokea nini?

8. **SFX:** **FIST HITTING TABLE LOUDLY**

9. **CHEUPE:** **(screams in fear)** Wooi, mbona unakakamaa! Pole basi. Nisamehe kama nimekukosea.

10. **KAPAKA:** **(breaking down to tears)** Haikuwa mimi…Ninaapa.
**(now crying uncontrollably)**

11. **CHEUPE:** **(Trying to comfort her husband)** Kapaka, ni sawa. Sijui kilichotokea lakini nakuamini mume wangu. Sijawahi kukuona katika hali hii, hapo awali. Kunitishia huku si kuzuri,hasa kwa mimba yangu. Sasa tulia unieleze, kumetokea nini?

12. **KAPAKA:** **(Bitterly)** Niache! Naomba uniache. Cheupe, tafadhali nahitaji muda wa kutafakari peke yangu. Nisamehe sijui nitakueleza vipi. Niache nitulie kwanza.

13. **CHEUPE:** Kapaka, ni majuzi tu tuliapa mbele ya mwenyezi Mungu na watu kuwa nitakuwa nawe wakati wote wa raha na shida, mbona leo usiniambie lililokufika? Mmmh, mimi ni mkeo sasa. Tunahitaji kusaidiana.

14. **KAPAKA:** La, Cheupe! Wewe jali kuhusu hali yako na ya mtoto. Mimi nitajishughulikia mwenyewe. Nisamehe, nahitaji muda niwe peke yangu.

15. **CHEUPE:** **(bewildered)** Lakini mpenzi…una…

16. **KAPAKA:** Unapopiga kelele zaidi unazidi kunikoroga. Kwani huelewi nisemacho? Ala! Nahitaji kupata lepe la usingizi. Labda litanituliza.

17. **SFX:** **SOMEONE LYING DOWN ON A BED WITH SPRINGS**

18. **MSIMULIZI:** Huku akiwa ameduwaa na mimba yake Cheupe alimtazama mumewe ambae daima ni mcheshi na mchangamfu, leo akilala bila hata ya kumsemesha . Swali akilini mwake ni: Kapaka amebadilishwa na nini? Huku tukimuacha akiwa amepotea kwenye lindi la mawazo, turudi chuoni, Valerie na Irene wako chumbani mwao baada ya kumaliza masomo siku hiyo.

**<u>SCENE TWO: VALERIE NA IRENE CHUMBANI MWAO</u>**

19. **ATMO:** **POPULAR LOCAL MUSIC PLAYING ON RADIO**

20. **IRENE:** **(singing along and dancing)** Val… Hebu, ingia kwenye miondoko! Usiwe hivyo. Hei.. unajua nini? Tunahitaji tujitumbuize. Twahitaji twende kilabuni, tucheze muzika hadi kunakucha, wasemaje?

**(music plays in background)**

21. **IRENE:** Valerie…una shida gani? Unafaa ufurahie kucheza muziki… uuuh… hebu.. – jitupe kwenye sakafu.

22. **VALERIE:** **(softly)** Zima redio.

23. **IRENE:** Ati? Sikukusikia vyema. zungumza, Val!

24. **VALERIE:** **(screams at the top of her voice)** Nimesema zima hiyo redio!!!

25. **IRENE:** **(caught by surprise)** Hei, sawa…hamna shida. Nakusikia.. kelele hizo ni za nini, kama mwenda wazimu?

26. **SFX:** **RADIO TURNED OFF**

**(absolute silence )**

27. **IRENE:** Haya hakuna muziki sasa… tufanyeje?

28. **VALERIE:** **(cuts her short )** Ssssh!

**(short silence)**

29. **VALERIE:** Wamefika. Wamekuja kunichukuwa!

30. **IRENE:** Valerie, wacha zihaka. Hakuna mtu yeyote hapa isipokuwa wewe na mimi. Umekuwa ukitumia kileo gani kwani? Chochote kile, ujuwe hakikufai.

31. **VALERIE:** **(out of her mind)** Hapana! Hamtanichukua...sitakubali! **(fearful)** usinikaribie …La! Niwacheni...

32. **IRENE:** **(shocked)** Oh jamani… Val, kumbe si mzaha.

Umerukwa na akili! Itanibidi nitafute msaada. Ninaishi na mwendawazimu, na mimi sina habari.

33. **VALERIE:** **(begging)** Tafadhali usiende. Ukiondoka watanichukua. Baki na mimi. Naogopa. Usiende tafadhali.

34. **IRENE:** **(scared)** Sawa, Valerie, basi niachilie mkono wangu, siendi, nakuahidi. Sawa, polepole niache mkono wangu.

35. **VALERIE:** Asante...

36. **SFX: IRENE IS QUICKLY STANDING UP AND LEAVES THE ROOM**

37. **SFX: DOOR QUICKLY BEING OPENED, CLOSED AND LOCKED**

38. **VALERIE:** **(totally frightened)** La!!!! Nifungulie, tafadhali nifungulie mlango...

39. **IRENE:** **(from outside the room while running away)** Nisaidieni! Jamani nisaidieni!!!

40. **MSIMULIZI:** Irene ametishika kweli na mwenendo wa Valerie, na sasa ameamua kutafuta msaada. Watu wengi wana ufahamu finyu kuhusu maradhi ya akili, hata wale walio katika nyanja za matibabu. Hofu na kutengwa kwao ni kwingi na ndio maana huwa hawapewi fursa ya kutibiwa. Ikiwa hawatafikiriwa kuwa mapepo basi wengi hufikiriwa kuwa wagonjwa hawa, walifanya tukio ovu ndipo sasa wamelaaniwa na kupata maradhi ya akili. Je, Valerie atapatwa na yapi sasa? Bado urafiki wake na Irene utadumu? Endelea kusikiliza upate jibu. Lakini kwa sasa, tumtembelee Chumba kule kijijini, kijana huyu anaugua maradhi ya akili, na sasa ana homa kali. Mamake, Malemba, anahofu zaidi na kumpeleka kliniki moja hapo mtaani. Huko wanakutana na nesi Matilda.

**<u>SCENE THREE: MALEMBA NA CHUMBA KATIKA KLINIKI YA MTAANI</u>**

41. **ATMO: CLINIC AMBIENCE (INCLUDING PEOPLE IN THE BACKGROUND)**

42. **MALEMBA:** **(desperate)** Samahani, mwanangu… anahitaji kumuona daktari, ana joto jingi mno. Nimefanya niwezavyo lakini hali inazidi kuwa mbaya.

43. **CHUMBA:** **(groaning in pain)** Aaargh... aarrgh... kichwa…

kichwa…

44. **MATILDA:** Umri wake?

45. **MALEMBA:** Chumba ana miaka 16. Nesi, tafadhali msaidie ana maumivu mengi.

46. **MATILDA:** **(shocked)** Miaka 16! Anaketi kama wa miaka saba! Mbona amedhoofika hivi? Anaumwa na nini tena?

47. **CHUMBA:** **(still in pain)** kichwa… kichwa… Mama… kichwa…

48. **MALEMBA:** Nesi, tafadhali tusaidie, kichwa kinamuuma sana. Husikii jinsi anavyolalamika!

49. **MATILDA:** Mama, kabla hajamuona daktari, nahitaji kujua rekodi yake ya matibabu. Nafikiri kuna kitu zaidi ambacho si cha kawaida kumhusu. Ana wazimu?... Namaanisha akili yake sio sawa?

50. **MALEMBA:** Chumba hana wazimu. Huvamiwa tu na mapepo wakati fulani fulani. Ni hayo tu.

51. **CHUMBA:** **(starts to make noises hard to understand)**

52. **MATILDA:** **(angrily)** Tafadhali mwambie aache kelele! Tuna wagonjwa wengine hapa. Sikiliza, samahani lakini

sidhani kama tunaweza kukusaidia. Kijana wako anahitaji tiba maalum na vifaa hivyo hatuna kwa sasa. Nakushauri umpeleke hospitali kuu jijini huenda ukasaidika huko.

53. **MALEMBA:** Kwa sasa nahitaji tu matibabu ya homa! Siwezi kumpeleka jijini kwa sababu sina fedha? Kumleta hapa tu nimembeba njia nzima. Nesi, lazima utusaidie. Tafadhali si unaona anavyotaabika.

54. **MATILDA:** Bila shaka namuona, lakini ni kama nilivyosema, hatutibu wenda wazimu hapa, tunatibu magonjwa madogomadogo ya kuja na kwenda hatuwezi kuwalaza wagonjwa hapa. Kijana wako anataka huduma ya hospitali ya malazi ya wenda wazimu.

55. **CHUMBA:** **(continues with his noises)**

56. **MATILDA:** Samahani, itawabidi mwende. Kijana wako anaogopesha wagonjwa wengine, muondoe kabla hajaleta maafa makubwa zaidi.

57. **MALEMBA:** Kijana wangu si hatari! Hatishii mtu yeyote.

58. **SFX: BABIES START CRYING IN THE BACKGROUND**

59. **MATILDA:** Hilo ndilo nisilolitaka. Haya muondoshe haraka. Kijana wako anafaa kuwa hospitali saa hizi.

60. **MALEMBA:** Kijana wangu si mwenda wazimu! Nikwambie mara ngapi? Njoo, Chumba, turudi nyumbani. Nitakupeleka kwa mganga wa kienyeji, Mizanja. Heri yeye ana utu.

61. **MSIMULIZI:** Malemba hakukosea. Hospitali nyingi barani Afrika hazina huruma na hazijali watu wanaougua maradhi haya ya akili. Utafiti umethibitisha kuwa, Guinea Bissau haina wataalamu wa akili wala washauri wa akili. Liberia ina mtaalam mmoja tu katika nyanja hii, na nchi nyinginezo hazina wataalam kabisa, ijapokuwa Shirika la Afya Duniani (World Health Organization) limekadiria kuwa asilimia 80 ya watu wanaougua maradhi ya akili wamo katika nchi zinazokuwa kimaendeleo, hivi sasa. Huku Malemba akibebana na mwanae Chumba kwenda kwa Mizanja, mtabibu wa kienyeji, Cheupe anazidi kushangazwa na tabia mpya za mumewe Kapaka.

**SCENE FOUR: KAPAKA AND CHEUPE AT HOME**

62. **SFX: SOMEONE SNORING HEAVILY**

63. **CHEUPE:** Kapaka! Kapaka! Amka. Tunahitaji kwenda kanisani, umesahau? Saa hii ni mchana, tena Jumatano, mazoezi ya uimbaji yataanza hivi punde.

64. **KAPAKA:** **(getting up)** Ah Cheupe, wewe nenda. Leo sina hamu. Tafadhali , uniombee udhuru kwa mwalimu wa kwaya.

65. **CHEUPE:** Kapaka, una uhakika! Unaniambia nidanganye kanisani? Ulipenda sana kuimba, imekuwaje? Au kwa sababu umepoteza kazi yako? Kapaka, ni wengi wasio na kazi na…

66. **KAPAKA:** Cheupe, sihitaji kuhubiriwa kwa sasa, wewe nenda. Nitakwenda juma lijalo.

67. **CHEUPE:** Niwaambie wanakwaya wakuombee? Unajua wakikuombea unaweza kupata hata kazi nzuri zaidi...

68. **KAPAKA:** Cheupe, fanya utakalo, nataka kulala kwa sasa...

69. **CHEUPE:** Hmm, leo umenishangaza mno, huli vizuri, ukilala unalala fofofo huamki, mwanzoni ulipenda sana kuimba lakini sasa hutaki hata kusikia wimbo. Una nini?

70. **KAPAKA:** Si kitu! Tafadhali nizimie taa na ushushe pazia, sihitaji mwangaza wowote.

71. **CHEUPE:** Ni saa tisa mchana. Giza litatoka wapi? unanitisha Kapaka… ninaanza kuwa na wasiwasi juu ya hali yako.

**<u>HITIMISHO:</u>**

Cheupe ana haki ya kupatwa na wasiwasi. Kapaka amebadilika, kwa lugha ya kitaalamu anaugua “ depression”, yaani sononi ama

mfadhako, tatizo linalowapata watu wengi. Hii ni hali gani? Na mambo ya Chumba na Valerie yataendeleaje? Kwa majibu ya maswali haya na mengineyo, usikose kusikiliza kipindi kifuatacho cha **“bado ningali mwanadamu”**, katika mfululizo wa hadithi hii inayoangazia matatizo wanayoyapata watu wanaougua maradhi ya akili barani Afrika. Ukitaka kusikiliza kipindi hiki au kingine kilichopita tembelea wavuti wetu, dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine, kwaheri.